# KANUNI ZA KUTAFSIRI BIBLIA

## DONDOO MUHIMU KUTOKA KWA MASOMO YOTE

shepherds
GLOBAL CLASSROOM

# Somo la 1 Dondoo Muhimu

(1) Sababu za Kujifunza Biblia:

- Mungu Amejifunua Mwenywe Kupitia Maandiko.
- Biblia ni Taa.
- Biblia ni Maziwa ya Kiroho.
- Biblia ni Asali Tamu.
- Biblia ni Upanga wa Roho.

(2) Zipo hatua tatu katika mchakato wa kujifunza Biblia.

- Uchunguzi: Ninaona nini katika Biblia? Jifunze:
    - Maneno
    - Muundo
    - Aina ya Fasihi
    - Mazingira
- Tafsiri: Biblia inamaanisha nini?
- Matumizi: Ni kwa namna gani ninaitumia Biblia katika maisha na huduma leo? Uliza:
    - Inafanyaje kazi kwangu?
    - Inafanyaje kazi kwa wengine?

(3) Tunatakiwa kuangaziwa na Roho Mtakatifu wakati tunajifunza Biblia. Kwa sababu hii

- Kujifunza kwetu kunatakiwa kutanguliwa na maombi.
- Ujifunzaji wetu wa Maandiko unatakiwa kufuatwa na mwitikio binafsi.

# Somo la 2 Dondoo Muhimu

(1) Anza mchakato wa Uchunguzi kwa kujifunza mstari mmoja. Jiulize maswali mengi kwa kadiri unavyoweza kuhusiana na mstari.

(2) Hatua za kukuza nguvu zako za uchunguzi zinajumuisha:

- Soma ili kupata uelewa.
- Uliza maswali unaposoma.
    - Nani?
    - Nini?
    - Lini?
    - Wapi?
    - Kwa nini?
    - Kwa namna gani?
- Soma kifungu cha andiko au kitabu hicho mara nyingi.
- Jifunze sarufi. Angalia:
    - Vitenzi
    - Majina
    - Vivumishi
    - Vishazi Vihusishi
    - Maneno Yanayounganisha
- Tafuta Taarifa Maalumu katika Andiko. Angalia:
    - Maneno yaliyorudiwa rudiwa
    - Ukinzani
    - Ulinganifu
    - Orodha
    - Tamko la kusudi
    - Vishazi Masharti
- Omba unaposoma.

# Somo la 3 Dondoo Muhimu

(1) Unaendelea na mchakato wa Uchunguzi kwa kusoma kifungu cha maandiko na kisha kitabu chote. Kwa asili, Biblia ilikuwa haijagawanywa katika sura na mistari. Ni lazima uhakikishe kwamba unafuata mgawanyo wa asili wa andiko katika kujifunza kwako.

(2) Unaposoma kifungu cha maandiko, angalia:

- Mahusiano ya jumla kwenda mahususi
- Sehemu za swali na jibu
- Mahojiano
- Toni ya kihisia

(3) Unaposoma kitabu chote, angalia:

- Mambo Yanayosisitizwa. Mwandishi anaweza kusisitiza mambo akijumuisha:
    - Kiwango cha Nafasi
    - Kusudi lililotamkwa
    - Mpangilio wa nyenzo
- Mambo Yaliyorudiwa Rudiwa
    - Maneno na vishazi vilivyorudiwa rudiwa
    - Watu waliorudiwa rudiwa
    - Matukio au mazingira yaliyorudiwa rudiwa
- Kuhama kwa Mwelekeo
- Muundo wa Uandishi
    - Muundo wa Kiwasifu
    - Muundo wa Kijiografia
    - Muundo wa Kihistoria au Kiwakati

(4) Kutengeneza jedwali katika sehemu ya maandiko au kitabu chote kunaweza kuelezea muundo.

# Somo la 4 Dondoo Muhimu

(1) Hatua ya tafsiri inauliza, "Andiko linamaanisha nini?"

(2) Baadhi ya changamoto zinazofanya tafsiri kuwa ngumu ni:

- Tofauti ya Lugha
- Tofauti ya Utamaduni
- Jiografia Isiyojulikana
- Aina ya Fasihi Isiyofahamika

(3) Baadhi ya makossa ambayo yanapelekea tafsiri isiyosahihi ni:

- Kusoma andiko kimakosa
- Kupindisha andiko
- Kutoa maana ya kufikirika

Kujiamini kupita kiasi

# Somo la 5 Dondoo Muhimu

(1) Tafsiri sahihi inahitaji kujifunza muktadha wa kila kifungu mahususi cha Biblia.

(2) Muktadha wa kihistoria-kiutamaduni unazingatia mazingira ya kitamaduni ya Biblia. Uliza:

- Tunafahamu nini kuhusiana na mwandishi wa Biblia?
- Tunafahamu nini kuhusiana na wapokeaji wa Biblia?
- Tunafahamu nini kuhusiana na mazingira ya kihistoria ya kitabu?
- Tunafahamu nini kuhusiana na mazingira ya kiutamaduni ya kitabu?

(3) Muktadha wa Biblia unaagazia ni kwa namna gani mstari unakaa vizuri katika andiko lote.

# Somo la 6 Dondoo Muhimu

(1) Tafsiri sahihi inatuhitaji sisi kuelewa aina ya fasihi ya kifungu cha maandiko tunachojifunza.

(2) Baadhi ya aina muhimu sana za fasihi zinazopatikana katika Biblia zinajumuisha:

- Historia: historia ya kweli na ya uhakika ya watu halisi na matukio halisi.

  Unapotafsiri historia, uliza:

  - Habari ni nini?
  - Watu katika habari ni nani?
  - Je, simulizi hii ya kihistoria inatoa mfano wa kufuata?
  - Je, ni kanuni gani zinazofundishwa katika simulizi ya kihistoria?

- Sheria za Agano la Kale

  Agano la Kale ni muhimu kwa ajili ya waamini wa Agano Jipya kwa sababu:

  - Ni maelezo ya asili ya Mungu.
  - Linatufanya sisi wenye hekima kwa ajili ya wokovu.
  - Linatusaidia kufahamu mapenzi ya Mungu.

  Inaweza kuwa ya masaada sana kufikiri kuhusiana na Nyanja tatu za Sheria za Agano la Kale:

  - Sheria za kiibada
  - Sheria za kiraia
  - Sheria za kimaadili

  Unapotafsiri Sheria za Agano la Kale, uliza:

  - Andiko hili lilimaanisha nini kwa wapokeaji wa kwanza?
  - Ni tofauti gani iliyopo baina ya wapokeaji wa Biblia na ulimwengu wetu?
  - Ni kanuni gani zinazofundishwa katika andiko hili?
  - Je, Agano Jipya linachukua kanuni hizi kwa namna yeyote?

- Ushairi

  Sifa za mashairi ya kiebrania:

  - Usambamba
  - Tamathali za semi

- Mashairi yenye hekima: yanafundisha namna maisha yanavyoenda.
- Mithali: uchunguzi wa jumla wa maisha umetajwa kwa ufupi na kwa uwazi.

  Unapotafsiri Mithali, uliza:

  - Ni kanuni gani za jumla zinazofundishwa katika andiko hili?
  - Je, ni hali gani za zisizo za kawaida zinazoweza kutokea katika kanuni hii?
  - Ni watu gani katika Biblia ni kielelezo cha kanuni hii?

- Unabii wa Agano la Kale: mawasiliano ya ujumbe kutoka kwa Mungu.

  Unapotafsiri unabii wa Agano la Kale, uliza:

  - Nabii alisema nini kwa ulimwengu wake?
  - watu wake waliitikiaje ujumbe wake?
  - Ni kanuni gani kutoka katika ujumbe wa nabii inayozungumza katika ulimwengu wetu leo?

- Fasihi ya kiapokaliptiki

  Unapotafsiri fasihi ya kiapokaliptiki, kumbuka:

  - Imejaa alama.
  - Sio lazima ielezee matukio katika mfuatano wa matukio
  - Inaweza kurudia kuelezea matukio yale yale kwa kutoa taarifa tofauti za kina.

  Dhana kuu katika fasihi ya kiapokaliptiki ni:

  - Changamoto ya kutunza imani katika ulimwengu huu wa uovu
  - Mungu Mwenyezi ambaye anasaidia watu wake.

- Mifano: mafundisho yanayolinganisha kweli ya kiroho na mambo katika asili au mazingira ya maisha. Mara nyingi mifano ilitolewa kama mwitikio ili kujibu swali au mtazamo.

  Unapotafsiri mifano, uliza:

  - Ni kwa namna gani mfano ulitolewa?
  - Hitimisho la mfano lilikuwa ni nini?
  - Ni mwitikio gani au mabadiliko gani ya mtazamo ambayo mfano unatoa?
  - Wapokeaji wa kwanza walikuwa na mwitikio gani?

- Waraka

  Nyaraka za Agano Jipya ni:

  - Zenye mamlaka
  - Za kimazingira
  - Zilielekezwa kwa waamini

  Unapotafsiri nyaraka, uliza:

  - Nani ni wapokeaji wa waraka?
  - Nani ni mwandishi? Anahusianaje na wapokeaji?
  - Ni mazingira gani yalipelekea kuandikwa kwa waraka?

- Ufafanuzi: mafundisho yenye mpangilio maalumu

# Somo la 7 Dondoo Muhimu

(1) Kujifunza neno ni kuchunguza maneno muhimu katika kifungu kwa makusudi ya kugundua maana yake ndani ya muktadha. Kujifunza neno kunatusaidia sisi kutafsiri kwa usahihi kifungu tunachojifunza.

(2) Makosa mawili yaliyozoeleka ya kuepuka unapofanya kujifunza neno:

- Kupuuza maana ya awali ya neno
- Kufikiri kwamba neno lina maana ile ile katika kila muktadha

(3) Mchakato wa kujifunza neno:

- Chagua neno la kujifunza.
  - Maneno ambayo ni muhimu kwa ajili ya maana ya kifungu
  - Maneno yaliyorudiwa rudiwa
  - Tamathali za semi
  - Maneno yasiyo wazi au ni magumu
- Orodhesha maana zinazowezekana kwa kila neno lililochaguliwa.
- Tambua kila neno lina maanisha nini katika muktadha wa kila kifungu.

(4) Maswali ambayo yatatusaida kutambua ni nini neno linamaanisha katika muktadha:

- Je kuna ukinzani au ulinganifu katika kifungu ambao unakusaidia kutoa maana ya neno?
- Ni kwa namna gani mwandishi ametumia neno hili katika maeneo mengine?
- Muktadha unaonesha nini kuhusiana na maana ya neno?

(5) Mambo ya kukumbuka unapojifunza lugha ya kitamathali:

- Wazo ambalo linawakilishwa ndiyo muhimu.
- Picha, kifungu cha maneno, au neno la kitamathali linawakilisha kitu kingine.
- Lugha ya kitamathli inataka umakini kwa sifa za kile inayokiwakilisha.
- Tunatakiwa kujaribu kuelewa andiko katika namna ambayo mwandishi alikusudia andiko kueleweka hivyo—ama maana ni halisi au ya kitamathali.

(6) Wakati gani tunatafsiri sentensi ya kimaandiko kitamathali:

- Wakati kifungu kinakuambia kufanya hivyo
- Wakati maana halisi haiwezekani au ni upuuzi

# Somo la 8 Dondoo Muhimu

(1) Uelewa wa kanuni za msingi za tafsiri ya Biblia utakusaidia kukuzuia kuja katika hitimisho lisilo sahihi katika kujifunza.

(2) Anza na andiko, na si hitimisho lako. Usiruhusu nadharia zako kukusababisha wewe kupuuza andiko.

(3) Mafundisho ya Maandiko hayakinzani na Mafundisho ya Maandiko. Kama vifungu viwili vinaonekana kukinzana, fikiri kwamba pengine haukuelewa vizuri mojawapo ya kifungu.

(4) Maandiko ni mtafsiri bora wa maandiko. Ruhusu vifungu vilivyo wazi kuelezea vifungu vigumu.

(5) Maandiko yaliandikwa ili kueleweka. Tafuta maana ya kawaida ya andiko.

(6) Maagizo ya Biblia yanaonesha ahadi za Biblia. Mungu anayetupatia maagizo anatuwezesha sisi kutii.

(7) Biblia ina maarifa yote yanayohitajika kwa ajili ya wokovu.

(8) Tunaangalia maandiko kupitia lenzi tatu ambazo zinatusaidia sisi kuelewa neno la Mungu:

- Utamaduni: uelewa wa wakristo wengine katika kipindi chote cha historia
- Mantiki: uelewa wa kimantiki wa andiko

Uzoefu: uzoefu wa kiroho wa wakristo

# Somo la 9 Dondoo Muhimu

(1) Haitoshi tu kwa sisi kutafsiri kwa usahihi Neno la Mungu; tunapaswa kulitendea kazi katika maisha yetu ya kila siku.

(2) Shetani anatujaribu sisi ili kuwa na mbadala wa matumizi:

- Tafsiri inakuwa mbadala wa Matumizi
- Utii Kwa Sehemu unakuwa mbadala wa Utii Kamilifu
- Tunafanya Visingizio kuwa Mbadala wa Toba
- Tunafanya Hisia kuwa Mbadala wa Kubadilishwa

(3) Ili sisi kufanyia kazi maandiko katika maisha yetu, tunatakiwa kufuata hatua hizi tatu:

- Fahamu maana ya andiko.
- Elewa ni kwa namna gani andiko linatumika katika maisha.
- Tii Maandiko.

(4) Ili kupata njia za kutendea kazi maandiko katika maisha yako, uliza maswali haya:

- Je, kuna dhambi ya kuepuka?
- Je, kuna ahadi ya kuidai?
- Je, kuna hatua ya kuchukua?
- Je, kuna Agizo la kutii?

Je, kuna mfano wa kufuata?